

ENDUIMET WMA

WMA ya Enduimet WMA ipo katika wilaya ya Longido, kaskazini magharibi mwa Mlima Kilimanjaro, na imeambaa mpaka mpakani mwa Kenya. Ilipata kibali rasmi cha kuwa WMA mwaka 2007, na ina vijiji tisa wanachama, ambavyo ni: Olmolog, Sinya, Kitendeni, Tinga Tinga, Elerai, Ngereiyani, Lerang'wa, Irkaswa, na Kamwanga. Wengi wa wakazi wake ni wafugaji wa Kimasai ambao mifugo yao huchungu pamoja na wanyamapori katika mbuga zenye ukame. Kuanzishwa kwa vikwazo vya malisho ya mifugo limekuwa ni suala lenye utata tangu utekelezaji wa WMA ulipoanza. Hadi sasa vijiji vya Enduimet vimefanikiwa kudumisha upatikanaji wa malisho ya mifugo. Makundi ya wanyamapori wanaohamama kati ya hifadhi ya taifa ya Kilimanjaro na Amboseli ya Kenya hupitia Enduimet. Kwa sababu hiyo, WMA hii huchukuliwa kuwa na umuhimu mkubwa katika hifadhi na utalii. Hivi sasa kuna mwekezaji mmoja katika sekta ya uwindaji, na vile vile kuna hoteli mbili na kambi moja ya kulala wageni. Mgogoro mkubwa kati ya WMA na moja ya hoteli na mwendeshaaji mmoja wa biashara ya utalii ulijikita zaidi katika vita vya kisheria, unahatarisha uwezo wa WMA kuzalisha mapato, licha ya kuwepo malalamiko ya mara kwa mara ya wakazi yanayopelekwa kwa Mbunge na serikali ya Wilaya.


Kuhusu Mradi wa Utafiti wa PIMA

Utafiti wa faida na athari zitokanazo na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za jamii (WMAs) kwenye mazingira na umaskini (PIMA) ni mradi wa utafiti wa kimataifa ulioendesha kwa ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha London, Chuo Kikuu cha Kopenihageni, Chuo Kikuu cha Imperial London, Chuo Kikuu cha Edinburgh, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Ufuatiliaji wa Uhifadhi Duniani, na Jumuiko la Maliasili Tanzania. PIMA ilikusanya taarifa za ngazi ya kaya kuhusu mali na hali za kimaisha kwa kutumia madodoso na kwa kuzipanga kaya katika madaraja tofauti ya kiuwezo (umiliki mali). PIMA pia ilikusanya taarifa katika ngazi ya kijiji na WMA kuhusu uendeshaaji wa WMA ikiwa ni pamoja na ugawanaji mapato. Taarifa hizi zilikusanywa katika vijiji 42 ndani na nje ya WMA sita zilizo kaskazini na kusini mwa Tanzania. Upangaji wa kaya katika madaraja ya kiuwezo ulifanyika kwa kaya zaidi ya 13,500. Dodoso zilitumika kukusanya taarifa kuhusu mali na mbinu za kimaisha kabla na baada ya kuanzishwa kwa WMA kutoka kwa wanaume na wanawake katika kaya zinazokaribia 2,000 (lengo ni kulinganisha hali ya maisha kati ya kipindi cha mwaka 2014-15 wakati wa utafiti wa PIMA na hali ilivyokuwa mwaka 2007 kulingana na kumbukumbu ya mhojiwa). Kwa kulinganisha mabadiliko ya hali ya maisha kabla na baada ya WMA kati ya vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA, athari za WMA kwa hali ya maisha zinaweza kujulikana (Kielelezo 2).

Mapato ya WMA ya Enduimet

- Mapato yatakanayo na tozo mbalimbali katika WMA yanapaswa kugagwanywa kulingana na Kanuni zinazosimamia Jumuiya za hifadhi za Wanyamapori za Jamii za mwaka 2008 na 2012 (Kielelezo Na. 3).
- Mgawo wa mapato ya utalii hutolewa kwa serikali kuu (*nyeupe*) na kwa halmashauri ya wilaya (*nyeupe*)
- Mapato yanayobaki hurudishwa kwa Jumuiya inayosimamia WMA ambayo inaweza kubakiza nusu ya mapato (*michirizi*) na kugawanya nusu nyingine kwa vijiji wanachama (kijivu mpauko)
- Kielelezo Na. 4 kinaonyesha kiasi halisi ambacho asasi ya kiraia ya Enduimet imepokea, imetumia na kile kilichogawawia kwa vijiji wanachama kati ya mwaka 2007-2015. Kiasi kingi kimetumika katika kugharamia shuguli za ofisi na uhifadhi, kilichobaki kiligawanywa kwa vijiji wanachama. Mapato ya mwaka kwa kila kijiji yaliongezeka kutoka dola za kimarekani 1,200 mwaka 2008 hadi dola za kimarekani 8,250 mwaka 2015.


Ramani ya WMA ya Enduimet




Kielelezo Na. 1: Ramani ya WMA ya Enduimet (Nyeupe). Mipaka ya vijiji imechorwa kutokan na taarifa za kijiografia za ramani za vijiji, taarifa za pointi za kijiografia za kuonesha eneo kutoka NBS, WWF, TANAPA. Imeandaliwa na J. Bluwstein.

Jedwali la taarifa Muhimu: WMA ya Enduimet

Wilaya	Longido
Vijiji Wanachama	9
Idadi ya Wakazi (Sensa, 2002)	17,585
Eneo	750 km ²
Mwaka wa usajili	2007
Jina la asasi ya kiraia	Enduimet
Mapato ya WMA [\$], mwaka 2014/2015	173,422



Kielelezo Na. 2: Mbinu iliyotumiwa na PIMA kuonesha mabadiliko yaliyosababishwa na WMA




Kielelezo Na. 3: Mgawanyo wa mapato kutokana na ada za uwindaji wa kitalii na utalii wa picha kulingana na Kanuni za Utalii wa Picha 2008 na Kanuni za Jumuiya za hifadhi za Wanyamapori za Jamii ya mwaka 2012.

* WMA inaweza kufanya makubaliano ya kuongeza kiwango cha ada, ambapo 100% ya kiwango cha ziada hubakia kwa WMA ** Ada kubwa kabisa kwa nyara hutozwa kwa aajili ya uwindaji wa Tembo: Kati ya dola za kimarekani 15,000 - 20,000, kutegemea na ukubwa wa meno ya Tembo. *** Hukusanywa na serikali kuu, na baadaye kugawanywa kwa WMA baada ya kukatwa kodi. Ada hizi ni pamoja na ada ya mikataba, ada ya kulaza wageni, ada ya kutembea eneo la WMA, ada ya kuingiza gari n.k.

- Kiji cha Sinya kilijiunga na WMA mwaka 2009 kwa kulazimishwa
- Kabla ya WMA, kijiji cha Sinya kilikuwa na mkataba mnono na mwekezaji wa biashara ya utalii, kikijipatia takribani dola za kimarekani 30,000 kwa mwaka kati ya mwaka 2002-2004 (Trench et al. 2009).
- Hata kwa kuzingatia mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya fedha, mapato ya sasa ya kijiji cha Sinya ni sehemu ndogo tu ya kile ambacho ingekipata kama mkataba wake wa zamani ungeendelea. Licha ya kuchangia ardhi kubwa, na kuwa na wanyamapori wengi Zaidi, kijiji cha Sinya kinapata mgawo sawa wa mapato ya jumla ya WMA kama vijiji vingine.
- Hii inabakia kuwa ndio sababu kubwa ya manung'uniko. Mvutano unakuzwa zaidi kutokana na mmoja wa wamiliki nyumba ya kulala wageni kukataa kufanya mkataba sahihi na WMA, na kushindwa kwa WMA na/au serikali kusimamia sheria.

- Vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA vilikuwa na mabadiliko sawa kwenye mapato yatokanayo na rasimali za kimazingira, mapato ya kuni (yaliongezeka) na mkaa (yalipungua) (kielelezo Na. 6)
- Mapato yatokanayo na vifaa vya kujengea yalipungua kwenye vijiji vya WMA na kuongezeka kwenye vijiji visivyo vya WMA. Matumizi ya mbaao, samaki na nyama ya porini hayakuripotiwa
- Ingawa mapato yatokanayo na rasimali za kimazingira yamebadilika, kanuni za upatikanaji wa rasilimali za kimazingira katika WMA ya Enduimet zinaoneka kutobalika (isipokuwa kwa mkaa)




Kielelezo Na. 4: Mapato na Matumizi ya Enduimet. Chanzo: Ripoti ya fedha ya WMA Enduimet kwa mwaka 2014.

Viwango vya thamani ya ubadilishaji fedha vimezingatia viwango halisi kwa kila mwaka

Mabadiliko ya Hali ya Maisha katika WMA ya Enduimet

Mali


- Kulingana na mitazamo ya wakazi, kaya za Enduimet zilipangwa katika makundi ya 'maskini sana' 'maskini' 'kawaida' na 'tajiri' kufuatana na kiwango cha mali kwa mwaka 2014 na kumbukumbu za umiliki mali kwa mwaka 2007
- Katika vijiji vya WMA, kaya chache kutoka kundi la 'maskini' zilijiongezea mali kati ya mwaka 2007 na 2014 kulinganisha na zile zisizo za WMA
- Katika vijiji vya WMA, kwa wastani, kaya chache zimeingia katika kundi la tajiri kati ya mwaka 2007 na 2014 kuliko zile za vijiji visivyo vya (Kielelezo Na 5)



Kielelezo Na 5: Mabadiliko ya mali kati ya mwaka 2007 na 2014.

Upatikanaji wa Maliasili na Mapato yatokanayo na Mazingira


- Katika utafiti huu, upatikanaji wa maliasili maana yake ni kiwango ambacho sheria na kanuni huzuia au husaidia kaya kupata kuni, fito, asali ya porini, vyakula vya porini n.k. kwa ajili ya matumizi au biashara.
- Mapato yatokanayo na mazingira imaaminisha mapato yatokanayo na ukusanyaji na/au uuzaji wa maliasili.




Kielelezo Na.6: Mapato yatokanayo na rasimali za mazingira kwa vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA kwa mwaka 2007 na 2014.

Mbinu za Kimaisha

- Shughuli zinazoegemea katika mazingira (kilimo, ufugaji, mazao ya porini) zilichangia 66% ya jumla ya mapato yote ya kaya za WMA ya Enduimet na 73% katika kaya zisizo za WMA (Kielelezo Na. 7). Mapato ya kimazingira kutokana na mazao ya porini yanajumuisha kuni, vifaa vya kujengea, mbaao, samaki, asali n.k.
- Machango wa shughuli zinazoegemea mazingira (kilimo, ufugaji, mazao ya porini) ulipungua kutoka mwaka 2007 hadi 2014 katika vijiji yvote, vya WMA na visivyo vya WMA (Kielelezo Na. 8)
- Katika kaya za WMA, misaada na malipo ya kufanya vibarua yalichangia zaidi katika pato la jumla kwa mwaka 2014 kuliko kwenye vijiji visivyo vya WMA.
- Uanzishwaji wa WMA unaweza kuwa umeleta vikwazo katika shuguli za kimaisha zinazotegemea maliasili (Ingawa bado zinachangia 2/3 ya pato la kaya) na kupelekea watu kuhamia kwenye shughuli za vibarua visivyotegemea ardhi, pamoja na kutegemea misaada.



Kielelezo Na. 7: Mchango (%) wa vyanzo mbalimbali kwenye pato la jumla (mzunguko mzima) katika vijiji vya WMA ya Makame na vile visivyo vya WMA kwa mwaka 2014



Kielelezo Na. 8: Mabadiliko ya mchango wa chanzo cha mapato kati ya mwaka 2007-2014 katika vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA

Hata hivyo, vijiji vya WMA ya Enduimet WMA (Wilaya ya Longido) vinaweza kuwa viliathiriwa Zaidi na ukame mawaka 2009 kuliko vijiji visivyo vya WMA (vingi vikiwa wilaya ya Monduli) na kusababisha kupungua kwa shughuli zinazoegemea mazingira (Goldman and Riosmena 2013).

Ardhi ya Kilimo


- Ardhi ya kilimo inapimwa kwa kulinganisha uwiano wa idadi na umri wa wanakaya, na inaripotiwa kwa kufuata uwiano wa ukubwa wa eneo na idadi ya watu wazima katika kaya, yaani 'uwiano kwa mtu mzima'¹
- Kwa wastani, wakazi wa vijiji vya WMA na visivyo vya WMA wanayo ardhi ya mashamba yenye ukubwa sawa (kwa kipimo cha uwiano wa mtu mzima) (WMA: ekari 0.65 kwa mtu mzima, zisizo WMA: ekari 0.56 kwa mtu mzima)
- Katika vijiji vya WMA, watu walikuwa na ardhi kubwa kidogo ya kilimo mwaka 2014 kuliko mwaka 2007 (ekari 0.59 kwa mtu mzima), wakati kwa vijiji visivyo vya WMA hakukuwa na mabadiliko

Ardhi ya Malisho

- Kwa Enduimet, wahojiwa 4 kati ya 10 walisema inawezekana kuchungia mifugo ndani ya eneo la WMA kwa vipindi fulani, 6 kati ya 10 walisema inawezeka nyakati zote kwa mwaka mzima
- Wahojiwa 3 kati ya 10 wa vijiji vya Enduimet wanaamini kuwa upatikanaji wa malisho ya mifugo umekuwa mgumu kuanzia mwaka 2007, lakini hawadhani kuwa mabadiliko hayo yanahusiana na WMA
- Katika vijiji visivyo vya WMA, wahojiwa 5 kati ya kila wahojiwa 10 walisema upatikanaji wa ardhi ya kungungia umekuwa mgumu

Mifugo


- Neno 'mifugo' linamaanisha wanyama wote wafugwao majumbani (bila kujumuisha kuku). Ili kurahisisha kulinganisha aina tofauti za wanyama na idadi (kama vile mbuzi, ndama na ng'ombe), PIMA inatumia kipimo kijulikancho kama 'kipimo cha mifugo'²
- Kwa wastani, kati ya ya mwaka 2007 na 2014 idadi ya mifugo kwa 'kipimo cha mifugo' kwa kaya kilipungua kwa karibu ya nusu katika vijiji vya Enduimet (kielelezo Na. 9).
- Kijiji cha Sinya kilipata madhara makubwa zaidi ya kupungua kwa idadi ya mifugo. 'Kwa kipimo cha mifugo', kwa wastani, hivi sasa kaya zinamiliki mifugo 72 pungufu kuliko mwaka 2007
- Kwa wastani, mabadiko ya idadi ya mifugo inayomilikiwa ni makubwa zaidi katika vijiji vya WMA kuliko vijiji visivyo vya WMA. Katika baadhi ya vijiji visivyo vya WMA, watu wanamiliki mifugo mingi zaidi (kwa kipimo cha mifugo) kuliko mwaka 2007, na vingine ni kigogo au hakuna hakuna mabadiliko.
- Ukame lilikuwa ndio tatitzo kubwa zaidi katika vijiji vya Enduimet: nusu ya kaya zilipoteza mifugo yao kutoka na ukame, hasa ukame mkali uliotokea mwaka 2009 (tizama Goldman and Riosmena 2013).




Kielelezo Na. 9: Idadi ya mifugo (kwa kipimo cha mifugo) inayomilikiwa na kaya za WMA na zisizo za WMA kati ya mwaka 2007 na 2014

Athari za Wanyamapori kwa Wakazi WMA ya Enduimet

- Athari za wanyamapori kwa wakazi ni pamoja na vifo na majeraha kwa binadamu na mifugo, uharibifu wa mazao na mali nyingine. Matukio haya husababisha hasara kubwa.
- Kuna utofauti mkubwa wa idadi kaya zilizokumbwa na uharibifu wa mazao katika vijiji vya WMA ya Enduimet (Kielelezo Na. 10)
- Kijiji cha Kitendeni kiliathiriwa zaidi, labda kwa sababu ardhi yake hutumiwa na wanyapori kuhama kati ya hifadhi ya taifa ya Kilimanjaro na Amboseli ya Kenya
- Kijiji cha Sinya ni kikame sana, na kaya zake zaidi zaidi ni za kifugaji (6% ya mapato yote hutokana na kilimo). Ni kaya nne tu zilizosema mazao yao yaliharibiwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita
- Kaya nyingi katika vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA ziliripoti kuwa viwango vya uharibifu wa mazao umebakia kuwa vile vile au kuongezeka tangia mwaka 2007. Hata hivyo, kaya chache zilisema kuwa uharibifu wa mazao umepungua kwa sasa
- Wastani wa thamani ya mazao yaliyoharibiwa kwa kaya, kwa kipindi cha miezi 12, ulikuwa wa kiwango cha juu sana kitika vijiji vya WMA kuliko vile visivyo wa WMA (Kielelezo Na. 11)
- Kaya za vijiji vya WMA pia zilikumbana zaidi na kadhia ya wanyama wakali wakamatao mifugo kiliko zile za vijiji visivyo vya: Kaya za WMA kwa wastani zilipoteza mifugo 1.6 (kwa kipimo cha mifugo), wakati kaya zisizo za WMA kwa wastani zilipoteza mifugo 1 (kwa kipimo cha mifugo) katika matukio ya hivi karibuni ya wanyapori kuvaia mifugo.



Kielelezo Na. 10: Wastani wa uwiano wa kaya za WMA (65%, kuondoa kijiji cha Sinya) na zisizo za WMA (69%) zilizokumbana na uharibifu wa mazao kutokana na uvamizi wa wanyamapori katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti.



Kielelezo Na. 12: Picha na J.Lund

Kielelezo Na. 11: Wastani wa hasara iliyotokana na uharibifu wa mazao kwa kaya katika vijiji vya WMA na visivyo vya WMA. Angalizo: Kiwango cha hasara kimekokotolewa kutokana na makadirio ya eneo lililoharibiwa, uzalishaji wa mazao, na makadirio ya pesa za mauzo ya mazao

Hitimisho

Kwa muonekano wa mwanzo, WMA ya Enduimet inatoa fursa bora kwa mpango wa jumuiya ya hifadhi ya jamii, ambapo jamii inaweza kunufaika na uhifadhi wa wanyamapori kutokana na fursa za utalii. Hata hivyo, sehemu kubwa ya mapato inachukuliwa na serikali kuu na utawala wa WMA, vikwazo vya WMA kwa jamii katika upatikanaji wa rasilimali muhimu, kutowachulia hatua wawekazaji wanaovunja sheria, na kuongezeka kwa matukio ya wanyamapori kuharibu mazao, kwa ujumla kunadhoofisha mafanikio ya WMA. Kijiji kimoja kiliweza kuingia moja kwa moja katika mkataba mnono na mwendesaji wa biashara ya utalii kabla ya WMA. Shughuli za kilimo haziwekani katika vijiji vinavyochangia ardhi kubwa kwenye WMA na kuwa na idadi kubwa wanayapori, hivyo wahisi kuwa si haki kugawana mapato kwa usawa na vijiji vinavyochangia ardhi kidogo na pia kuwa wanyamapori wachache kwa vile wana fursa nyingine ya kuendesha shughuli za kilimo nje ya maeneo ya WMA. Athari za ukame wa mwaka 2009 katika idadi ya mifugo inayomilikiwa zilikuwa kubwa kuliko zile za WMA.

Kumbumbuku Rejea

¹Katika matokeo haya, ardhi ya kilimo imehusianishwa na idadi ya watu katika kaya, jinsia na umri, kwa sababu wanaume, wanawake, na watoto wa umri tofauti huhitaji kiwango tofauti cha chakula, na hivyo ukubwa sawa wa ardhi humanisha uwezo tofauti wa kutosheleza mahitaji kwa kaya mbalimbali. Kwa kutumia mfumo sanifu, tunawajumlisha wanakaya na kuwaweka katika kipimo cha 'uwiano wa mtu mzima', ambacho ni rahisi kulinganisha umiliki wa ardhi ya kilimo na mahitaji kwa kaya.

²Kama ambavyo PIMA imetumia mfumo sanifu wa uwiano wa mtu mzima, tunatumia 'kipimo cha mifugo' ili iwe rahisi kulinganisha makundi ya mifugo yanayoundwa kwa aina na ukubwa tofauti wa mifugo na mahitaji yao tofauti ya chakula. Kipimo kimoja cha mifugo ni sawa na ng'ombe mmoja mkubwa wa kilo 250kg. Mbuzi au kondoo kwa mfano, anahesabiwa kuwa sawa na moja ya kumi ya ng'ombe.

Shukrani

PIMA inawashukuru wakazi wa vijiji vya Olmolog, Sinya, Kitendeni, Tinga Tinga, Selela, Ortukai na Ngabobo, na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Enduimet kwa kushiriki katika utafiti huu. Mradi wa utafiti wa PIMA umefadhiliwa na ESPA: Mpango wa Utafiti wa Mazingira na Kuondoa Umaskini. ESPA inaendeshwa kwa pamoja na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Baraza la utafiti wa Mazingira (NERC) na Baraza la Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRC). Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti hii: www.ucl.ac.uk/pima

Jarida hili limeandaliwa na S. Funk kutokana na takwimu zilizokusanywa na mradi wa utafiti wa PIMA. A. Keane, M. Reinhardt Nielsen, J. Friis Lund, J. Bluwstein and K. Homewood kwa pamoja waliandaa mbinu za kukusanya, kuchambua na kutafsiri takwimu za PIMA. J. Olila aliongoza kikundi cha wakusanya takwimu. M. Msuha and N. Burgess walijihulikia takwimu za wanyamapori. V. Corey Wright anashurikuliwa kwa maoni yake.

Marejeo

Goldman, M. J. & Riosmena, F. 2013. Adaptive capacity in Tanzanian Maasailand: Changing strategies to cope with drought in fragmented landscapes. *Global Environmental Change*, 23, 588-597

Trench, P.C., et al., 2009, Still 'people of cattle'? Livelihoods, diversification and community conservaion in Longido District, in K. Homewood, P. Kristjanson and P.C. Trench, eds, *Staying Maasai? Livelihoods, Conservation and Development in East African Rangelands*, New York: Springer

WWF (2014): Tanzania's Wildlife Management Areas, 2012 Status Report



Mawasiliano: K. Homewood, Chuo Kikuu cha London, Idara ya Anthropologia. k.homewood@ucl.ac.uk